

02 - Historia Ya Elimu Ya Tajwiyd Na Viraa-a

Huenda msomaji akauliza: Je, Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) alisomewa na Jibriyl (عليه السلام) naye aliisoma Qur-aan kwa Tajwiyd? Na je, vipi au wakati gani imeanza kusomwa kwa kufuata hukmu za Tajwiyd?

Jibu ni kwamba, kusoma Qur-aan kwa Tajwiyd kulianza tokea ilipotemshwa Qur-aan, kwa maana: Jibriyl (عليه السلام) alimsomea Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) Qur-aan kwa Tajwiyd, kisha naye Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) akawasomea Maswahaba zake namna ile ile alivyosomewa na Jibriyl (عليه السلام), na Maswahaba kwa upande wao pia wakawasomea Taabi'iyina¹ kama walivyosomewa na Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم).

Wakati huo, Sayansi ya elimu ya Tajwiyd na hukmu zake hazikuwa zimeandikwa kinadharia, kwa kuwa walikuwa kila wakisoma Qur-aan huwa wanaisoma kama walivyosomewa bila hata kuhisi kuwa walikuwa wakifuata taratibu zilizokuja kueleweka na kuwekewa fani yenye kueleweka kama ni Sayansi ya elimu ya Tajwiyd.

Baada ya hapo dola ya Kiislamu ilipanuka, jambo lililopelekea watu wengi wa lugha na lahaja mbali mbali kuingia katika Uislamu na kutaka kusoma Qur-aan kama ilivyotemshwa.

Khofu ikawaingia Fuqahaa wa Qur-aan wa wakati huo kwamba Qur-aan itakuja kusomwa kinyume na ilivyotemshwa kwa kuwa hakuna taratibu wala kanuni zilizoandikwa ambazo zingeudhibiti usomaji wake. Pia Qurraa-a hawakuwa wenye kupatikana kila mji katika miji ya Waislamu. Hapo ndipo ilipoonekana kuwa kuna haja na umuhimu wa kuweko maandishi yatayodhibiti taratibu zenye kuudhibiti usomaji wa Qur-aan.

¹ Ni wingi wa Taabi'iy au Taabi' naye ni yule aliyekutana na Swahaba yeyote yule hali ya kuwa ni Muislamu na akafariki juu ya Uislamu.

Sayansi ya Tajwiyd ikaanzishwa na Fuqahaa wa Qur-aan, kwa njia ya kuorodhesha na kuandika kila hukmu katika hukmu zenye kufungamana na usomaji wa Qur-aan kama ilivyoteremshwa; hukmu ambazo zilichomolewa na kuchotwa kutokana na usomaji wa Qurraa-a ambao wamethibiti kuwa walipokea usomaji wao kutoka kwa Swahaba (رضي الله عنهم) ambao wamepokea kutoka kwa Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم). Kisha wakakabidhiwa wakufunzi mahiri jukumu la kizifundisha hukmu hizi kwa kila mwenye kutaka kuisoma Quraan kama ilivyoteremshwa.

Viraa-a ni *alfaadhwa* (matamshi) za visomo vya Qur-aan tukufu vinavyotoka katika madhehebu tofauti ya *nutwq'* (jinsi ya kuitamka) Qur-aan. Qaariu anachukua kisomo chochote kati ya Viraa-a hivyo ambavyo vyote vimethibiti kwa mapokezi Swahiyh kutoka kwa Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم). Kila Qiraa-a kina hukmu zake (Tajwiyd) za usomaji na hutofautiana katika baadhi ya maneno, herufi, *i'raab*, tamshi, kutangulia neno au kulichelewesha n.k kutokana na Herufi Saba² zilizothibiti. Kisha Qiraa-a kikapewa jina kutokana na Mwalimu maarufu wa Qiraa-a hicho. Mfano Qiraa-a tunachosoma sisi kinatokana na *Riwaayah* ya Hafsw³.

Na mtu wa kwanza anaetambulika au kukubalika kuwa amekusanya Viraa-a katika kitabu ni Abuu 'Ubayd Al-Qaasim ibn Sallaam (158/224H)⁴ ambaye

² Rejea Mlango Wa Herufi Saba Na Viraa-a Saba.

³ Jina Lake: Hafsw ibn Sulaymaan bin Al-Mughhiyrah bin Abiy Daawuwd, Al-Asadiyy Al-Kuwfiy. Kun-ya yake ni Abuu 'Amr.

Kazaliwa mwaka 90H. Kafariki 180H.

Hafsw ni mwana wa kambo wa 'Aaswim. Alijifunza Qur-aan kwa *talaqqiy* kutoka kwa baba yake 'Aaswim akawa bingwa wa Qiraa-a cha 'Aaswim. Alijifunza na kurithi elimu ya Qiraa-a akaisoma alipokwenda Baghdaad na Makkah. Amesifiwa na 'Ulamaa wa zama zake kuhusu umahiri wake wa fani ya Qur-aan kwa ujumla na khasa jinsi ya kutamka herufi zake na jinsi alivyoithibitisha, kikajulikana Qiraa-a chake kwa jina la "*Riwaayatu Hafsw 'an Aaswim.*"

⁴Abu 'Ubayd Al-Qaasim bin Sallaam Al-Baghdaadiy.

Kazaliwa katika Harraa katika mwaka wa 158H na baba yake alikuwa mtumwa wa Kirumi kwa baadhi ya watu wa Harraa.

Alikuwa ni Imaam, *Mujtahid*, bahari ya elimu, mwanaisimu na *Faqiyh* Alipokea elimu yake kutoka kundi la Imaam wa kuaminika, kama Sufyaan ibn 'Uyaynah,

aliwakusanya ndani yake Qurraa-a ishirini na tano kama ilivyokuja katika kitabu cha *An-Nashr fil-Qiraatil-'Ashr* cha Muhammad ibnil-Jazariyy.

Viraa-a Swahiyh vilivyopokewa kwa njia ya *Mutawaatir* ni kumi kwa *Riwaayah* ishirini ambazo hadi leo vipo na vinasomwa katika maeneno tofuati duniani. Saba katika hivyo, vimenukuliwa na Imaam Abuu Bakr ibn Mujaahid katika Kitabu chake na ambavyo vimetajwa katika Shairi maarufu la Ash-Shaatwibiyyah. Orodha ya Qurraa-a kumi na Raawiy (wanafunzi) wao mashuhuri ni kama ifuatavyo.

01) Naafi' Al-Madaniy: Naafi' ibn 'Abdir-Rahmaan ibn 'Abiy Na'iym Al-Laythiy. (70 - 169 H). Amezaliwa Madiynah alifariki akiwa na umri wa miaka 99.

Wanafunzi (Raawiy) Wake Mashuhuri waliohifadhi Qiraa-a chake ni:

i. **Qaaluwn:** 'Iysaa ibn Minaa Az-Zarqiy (120 - 220 H). Alikuwa ni mwana wa kambo wa Naafi' na aliishi maisha yake yote Madiynah. Baada ya kufariki Naafi' alichukua sehemu yake kama ni Qaariu mkuu wa Madiynah.

ii. **Warsh:** Abuu Sa'iyd 'Uthmaan ibn Sa'iyd Al-Miswriy (110 - 197 H). Aliishi Miswri akasafiri kuelekea Madiynah mwaka 155H kusoma chini ya Imaam Naafi'. Kisha akarudi Miswr akawa Qaariu mkuu wa Miswr.

Ismaa'iyil ibn Ulayyah, Yaziyd ibn Haaruwn, Yahya ibn Sa'iyd Al-Qattwaan, 'Abdur-Rahmaan ibn Mahdiy, Hamaad ibn Salmah na wengine.

Miongoni mwa vitabu vyake vinginevyo ni: '*Fadhwaail-Al-Qur-aan*' na '*Ghariyb Al-Hadiyth*.' Imaam Ad-Daarimiy, Abuu Bakr ibn Abiy Ad-Dun-yaa, 'Aliy ibn 'Abdil-Aziyz Al-Baghaawiy, Muhammad ibn Yahya Al-Marwaziyy na wengine wamepokea elimu kutoka kwake.

Abu 'Ubayd (رحمه الله), aliishi Baghdaad kwa muda, kisha akawa Qadhwi wa Turtuws, baada ya hapo aliamia Makkah na aliishi huko hadi alipofariki mnamo mwaka 224H.

Miongoni mwa kauli zake Abu 'Ubayd (رحمه الله) ni: "Mfuasi wa Sunnah ni kama yule ashikaye kaa la moto, na leo hii ni bora zaidi mbele ya macho yangu kuliko mwenye kushika upanga katika njia ya Allaah."

02) Ibn Kathiyr Al-Makkiy: ‘Abdullaah ibn Kathiyr Ibn ‘Umar Al-Makkiy (45 - 120 H). Alikuwa ni Taabi’ aliwahi kukutana na Maswahaba kama Anas ibn Maalik na ‘Abdullaah bin Zubayr.

Wanafunzi (Raawiy) Wake Mashuhuri waliohifadhi Qiraa-a chake ni:

i. **Al-Bazziy:** ‘Abdul-Hasan Ahmad ibn Bazzah Al-Makkiy (170 - 250 H). Alikuwa ni Muadhini wa Masjid Al-Haram Makkah na Qaariu mkuu Makkah kipindi chake.

ii. **Qumbul:** Abuu ‘Amr Muhammad ibn ‘Abdir-Rahmaan (195 - 291.H). Alikuwa Qaariu mkuu wa Hijaaz.

03) Abuu ‘Amr Al-Baswriy: Zab’aan ibn Al-‘Alaa ibn ‘Ammar Al-Baswriy: (69 - 154 H). Alizaliwa Makkah, akakulia Baswrah.

Wanafunzi (Raawiy) Wake Mashuhuri waliohifadhi Qiraa-a chake ni:

i. **Ad-Duwriy:** Hafsw ibn ‘Umar Ad-Duwriy (195 - 246 H). Alikuwa wa kwanza kukusanya Viraa-a mbalimbli juu ya kuwa alikuwa kipofu.

ii. **As-Suwsiy:** Abuu Shu’ayb Swaalih ibn Ziyaad As-Suwsiy (171 - 261 H). Alimfunza Qur-aan Imaam An-Nasaaiy.

4) Ibn ‘Aamir Ash-Shaamiy: ‘Abdullaah ibn ‘Aamir Al-Yahswabiy: (21 - 118 H). Aliishi Dimishiq (Damascus). Alikutana na baadhi ya Maswahaba akasoma Qur-aan kwa Maswahaba; Abuu Dardaa, Al-Mughhiyrah ibn Abiy Shihaab. Alikuwa Imaam wa Masjid Umayyad (Damascus) kipindi cha Ukhalifa wa ‘Abdul-‘Aziyz. Alikuwa mashuhuri kutokana na Qiraa-a chake.

Kati ya Qurraa-a saba, yeye ndiye aliyekuwa na Raawiy zaidi kulikoni wengineo.

Wanafunzi (Raawiy) Wake Mashuhuri waliohifadhi Qiraa-a chake ni:

i. **Hishaam:** Hishaam ibn 'Ammar Ad-Dimishiqiy (153 - 245 H). Alikuwa maarufu kutokana na Qiraa-a chake na ilmu yake ya Hadiyth na Fiqh na alikuwa mwalimu mmojawapo wa Imaam At-Tirmidhiy.

ii. **Ibn Dhakwaan:** 'Abdullaah ibn Ahmad Dhakwaan (173 - 242 H) Naye alikuwa pia ni Imaam wa Masjid Umayyad kipindi hicho.

5) **'Aaswim Al-Kuwfiy**⁵: 'Aaswim ibn Abiy Najuwd Al-Kuwfiy: (127 - 180 H). Alikuwa ni Taabi'. Alikuwa ni mwenye ilmu zaidi ya Qiraa-a kipindi chake.

⁵ Jina lake: 'Aaswim ibn Abiy An-Najuwd Al-Kuwfiy. Kun-ya yake ni Abuu An-Najuwd

Laqab yake ni 'Aaswim ibn Bahdalah kutokana na jina la mama yake.

Kafariki 127H Kufah.

Alikuwa ni miongoni mwa *Taabi'iyna*. Kushikamana kwake na Qur-aan kulitokana na nyayo za walimu waliohifadhi Qur-aan ambao wote waliathirika na Hadiyth ya Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) aliposema:

((خَيْرُكُمْ مَنْ تَعَلَّمَ الْقُرْآنَ وَعَلَّمَهُ)) صحيح البخاري

((Mbora wenu ni yule mwenye kujifunza Qur-aan kisha akaifundisha)) [Al-Bukhaariy]

Hadiyth hii imepokewa na 'Uthmaan bin 'Affaan ambaye naye akamhadithia mwanafunzi wake Abuu 'Abdir-Rahmaan As-Sulamiy (aliyefariki 75H) ambaye naye akapania kuitumikia na kuifundisha Qur-aan kwa miaka katika mji wa Kufah.

Miongoni mwa wanafunzi wa Abuu 'Abdir-Rahmaan As-Sulamiy ni 'Aaswim. Alipofariki As-Sulamiy, 'Aaswim alirithi kutoka kwake bahari ya elimu ya Qur-aan na uimamu wa Qur-aan. Mwanafunzi akawa mwalimu na akaendelea kufundisha.

Wanafunzi (Raawiy) Wake Mashuhuri waliohifadhi Qiraa-a chake ni:

i. **Shu'bah:** Shu'bah ibn Iyaash Al-Kuwfiy (95 – 193 H.)

ii. **Hafsw:** Abuu 'Amr Hafsw ibn Sulaymaan Al-Asadiy Al-Kuwfiy (90 – 180 H) Alikuwa mwana wa kambo wa 'Aaswim. Alikuwa ni mwenye ilmu zaidi ya Qiraa-a cha 'Aaswim.

6) **Hamzah Al-Kuwfiy:** Hamzah ibn Habiyy Al-Kuwfiy (80 – 156 H). Alikutana na baadhi ya Maswahaba. Isnaad ya Qiraa chake kinafikia kwa Nabiyy (صلى الله عليه وآله وسلم) kupitia kwa 'Aliy ibn Abiy Twaalib (رضي الله عنه) na 'Abdullaah ibn Mas-'uwd (رضي الله عنه).

Wanafunzi (Raawiy) Wake Mashuhuri waliohifadhi Qiraa-a chake ni:

i. **Khalaf:** Khalaf ibn Hishaam Al-Baghadaadiy (150 – 227 H). Alihifadhi Qur-aan alipokuwa na umri wa miaka kumi.

ii. **Khallaad:** Abuu 'Iysaa ibn Khaalid Ash-Shaybaaniy (119 - 220 H)

7) **Al-Kisaa'iy:** 'Aliy ibn Hamzah ibn 'Abdillaah (120 – 189 H). Alikuwa mwenye ilmu, mtaalamu mkubwa wa sarufi ya lugha ya Kiarabu. Aliandika

Miongoni mwa sifa zake ni kwamba alikuwa ni faqihi wa lugha na alikuwa na ufundi wa Qiraa-a kwa sauti nzuri mno. Alikuwa pia ni mwenye msimamo madhubuti wa Sunnah na aliaminika katika mapokezi ya Hadiyih.

Miongoni mwa wanafunzi wake ni Imaam Abuu Haniyfah, Imaam Ahmad ibn Hanbal ambaye aliulizwa siku moja. "Qiraa-a gani unapendelea kukisoma?" Akajibu: "Qiraa-a cha Madiynah (yaani cha Naafi') au sivyoyote cha 'Aaswim."

vitabu vingi, na akawa mtaalamu katika sayansi ya Qiraa-a. Khaliyfah Haaruwn Rashiyd alimheshimu mno.

Wanafunzi (Raawiy) Wake Mashuhuri waliohifadhi Qiraa-a chake ni:

- i. **Al-Layth:** Layth Ibn Khaalid Al-Baghdaadiy alifariki 240 A.H.
- ii. **Ad-Duwriy:** Ni Ad-Duwriy yule yule (Hafsw ibn 'Umar Ad-Duwriy (195 - 246 H) ambaye ni mwanafunzi wa Abuu 'Amr Al-Baswriy aliyetajwa juu, kwani alisoma akahifadhi Viraa-a vyote.

Hao ndio Qurraa-a saba Mashuhuri na wote hao walikuwa si Waarabu isipokuwa Ibn 'Aamir and Abuu 'Amr.

8) Abuu Ja'far Al-Madaniy: Yaziyd ibn Al-Qa'qa' Al-Makhzuwmiy. Alifariki mwaka 130 H. Alikuwa ni Taabi'. Alikuwa miongoni mwa walimu wa Imaam Naafi'.

Wanafunzi (Raawiy) Wake Mashuhuri waliohifadhi Qiraa-a chake ni:

- i. **'Tysaa ibn Wardaan.** Alifariki mwaka 160 H.
- ii. **Sulyamaan ibn Jamaaz.** Alifariki 170 H.

9) Ya'quwb Al-Baswriy: Ya'quwb ibn Is-haaq Al-Hadhramiy Al-Baswiry. Alifariki mwaka 205 H.

Wanafunzi (Raawiy) Wake Mashuhuri waliohifadhi Qiraa-a chake ni:

- i. **Ruways:** Muhammad ibn Mutawaakil. Alifariki mwaka 238H.

ii. **Ruwḥ:** Ruwḥ ibn ‘Abdil-Muumin Al-Baswriy. Alifariki mwaka 235H. Alikuwa miongoni mwa mwalimu wa Imaam Al-Bukhaariy.

10) Khalaf Al-‘Aashir: Alikuwa na Qiraa-a chake makhsusi cha aina ya pekee na alikuwa akiitwa ‘Khalaf Al-‘Aashir’ (Yaani Khalaf wa kumi) ili kumbainisha kuwa ndiye yule yule Khalaf aliyekuwa mwanafunzi wa Imaam Hamzah.

Wanafunzi (Raawiy) Wake Mashuhuri waliohifadhi Qiraa-a chake ni:

i. **Is-haaq:** Is-haaq ibn Ibraahiym ibn ‘Uthmaan. Alifariki mwaka 286H.

ii. **Idriys:** Idriys ibn ‘Abdil-Kariym Al-Baghdaadiy. Alifariki mwaka 292H.

Hata hivyo, Viraa-a vyengine si mashuhuri sana isipokuwa kwa *Mutakhasw-swiswawn* (watu walioshughulika zaidi) katika fani hii ya *Qiraa-a*, na vyengine ni mashuhuri sana, ambavyo pia vinazidiana kwa umashuhuri; navyo ni:

a-Hafsw ‘An Aaswim:

Asilimia zaidi ya 90 ya Waislamu Asilimia zaidi ya 90 wa Waislamu duniani wanasoma kwa Riwaaya hii, wakijumuika na Waislamu wa Afrika Mashariki na Bara Hindi.

b-Warsh ‘An Naafi’:

Kinasomwa zaidi Algeria, Morocco, sehemu za Tunisia, Afrika Magharibi, Sudan.

c- Qaaluwn ‘An Naafi’

Kinasomwa zaidi Libya, Tunisia, na sehemu za Qatar.

d- Ad-Duwriy 'An Abiy 'Amr

Kinasomwa zaidi Sudan na Afrika Magharibi.

e-Ibn 'Aamir

Kinasomwa zaidi sehemu fulani za Yemen.